

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

UFAHAMU (Ala.10)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Wanasayansi wengi wameshindwa kuelewa ni kwa ini watu huvuta sigara. Jambo hili limewatatiza binadamu kwa karne nyingi zilizopita na kuwacha rundo la maswali kuhusu uvutaji sigara.

Sigara au sigareti ni kitu cha **uraibu** wa kuvuta, kinachotengenezwa kwa majani ya tumbako yaliyokaushwa. Husokotwa katika karatasi maalum. Tumbako pia huvutwa kwenye kiko, hunuswa na hutafunwa. Tumbako inayosagwa na kunuswa au **kubwiwa** huitwa ugoro.

Hapana shaka uvutaji sigara huharibu afywa yao. Wataalamu wa sayansi na madaktari wamefanya uchunguzi na wamethibitisha kuwa moshi wa sigara huathiri wavutaji wa sigara na watu walio karibu nao nap engine huleta ugonjwa wa moyo. Wavutaji hupatawa na kikohozi cha daima kisichosikia dawa; mwishowe hupata maradhi mfano wa pumu kutokana na moshi wa sigara **unaowakereketa** koo. Kuna pia wanaosema kwamba uvutaji sigara unasababisha saratani ya mapafu. Watu wengi hufa kwa ugonjwa wa ghafla kwa sababu ya sumu ya moshi wa sigara ambao **hutaunguza** na kuyatoboatoboa mapafu.

Baadhi ya wavuta sigara hutupa vipande vya sigara ovyo bila kuzimwa na hivyo husababisha hasara kubwa kama vile uchomaji wa mistitu, nyumba na nguo na wakati mwingine husababisha hata vifo uvutaji sigara umefika kiwango cha kusikitisha. Utaona vijana, yaani wasichana kwa wavulana wadogo sana, wakivuta sigara mbele ya watu wazima bila kujali. Hii ni aibu kubwa sana.

Tabia hii inatokana na mifano wanayoiona kutoka kwa wazazi wao au watu wengine. Si ajabu kumsikia mzazi akimtuma mwanawe akamnunulie pakiti ya sigara au kopo la tumbako. Wazazi kama hao huwafanya watoto wao wavute sigara ili nao wajione kama ni watu wazima.

Sababu nyingine ya kuvuta sigara ni kutaka ahari ya kutaka kujionyesha ati wana nakidi na kwao, huo umaarufu. Hivyo basi, sigara hazifai kupatiwa matangazo yenye kuvutia kwa vijana.

Aina nyingine ya uraibu ni uvutaji bangi. Bangi ni aina yam mea Fulani unaolevya na kupumbaza akili yanapotafunwa au kuvutwa. Wavuta bangi kwa hakika hupatawa na baa nyingi mwilini, kukonda na huvirinagika akili wasijue wanalofanya. Wataalamu husema bangi ikiingia akilini, huharibu kituo cha fikira mpaka mtu huwa kama mwendawazimu.

Ni muhimu wazazi na walimu wawakataze na wawakanye watoto wasishiriki katika tabia hizi mbaya.

Maswali

1. Ipe taarifa uliyosima kichwa mwafaka (Ala.1)
Uraibu
2. Taja hasara katika mazingira ya mvutaji zinazosababishwa na uvutaji sigara (Ala.2)

- ✓ **Husababisha ugonjwa wa moyo**
- ✓ **Mtu hupata kikohozi cha daima kisichosikia dawa**
- ✓ **Hupata maradhi, mifano pumu**
- ✓ **Moshi wa sigara hukereka koo**
- ✓ **Husababisha iri/saratani ya mapafu**
- ✓ **Huyaumiza na kuyatoboatoboa mapafu**

3. Taja magonjwa yanayoletwa na uvutaji wa sigara (Ala.2)
- ✓ **Maradhi, mfano wa pumu**
 - ✓ **Kikohozi kisichokauka**
 - ✓ **Iri/saratani ya mapafu**
 - ✓ **Kuathirika kwa mapafu**
 - ✓ **Ugonjwa wa moyo**
4. Toa sababu mbili zinazoonyesha kwa nini vijana wa siku hizi huvuta sigara (Ala.2)
5. Eleza hatua mwafaka zinazofaa kuchukuliwa ili kukomesha viajana kuvuta sigara (Ala.3)
- ✓ **Sigara zisipatiwe matangazo ya kuvutia**
 - ✓ **Wazazi wasiwatume watoto wao madukani kuwanunulia sigara**
6. Eleza tofauti ya sigara, tumbako na bangi (Ala.2)
- Sigara – uraibu usiolewesha unaovutwa moshi ndani ya mapafu.**
- Bangi – uraibu usio halali wenye kulewesha au kupumbaza akili unapotafunwa au kubwiwa mdomoni.**
7. Fafanua maana ya misemo ifuatayo kama vilivyotumiwa katika taarifa (Ala.2)
- a) Kisichosikia dawa
- ✓ **Kisichotibika/kisichopona**
- b) Rundo la maswali
- ✓ **Maswali mengi**

MATUMIZI YA LUSHA (Alama 25)

- a) Eleza maana ya silabi (Ala.1)
- ✓ **Pigo la sauti katika neon**
 - ✓ **Tamka kamili katika neno**
- b) Toa tofauti kati ya silabi mwabatana na sauti mwambatano (Ala.2)
- ✓ **Silabi mwambatano – ni mfuatano wa konsonanti mbili au tatu pamoja na irabu – (KKKI)**
 - ✓ **Sauti mwambata – ni konsonanti mbili au Zaidi zinazotamkika kama sauti moja.**

c) i) Mofimu ni nini?

✓ **Ni kipashio kidogo kabisa chenye maana kisarufi**

ii) Taja aina za maofimu na utoe mfano moja moja

✓ **Mofimu huru – mfano (mimi,darasa)**

✓ **Mofimu tegemezi, funge – (M-Mtu, Aliyempiga)**

(Ala.2)

d) Eleza maana tatu ya sentensi hii

(Ala.3)

i) **Kewa niaba**

ii) **Kuelekea kwake**

iii) **Kwa sababu**

iv) **Mpira kama kitaa**

e) Tambua vielezi mbali mbali ya namna au jinsi

(Ala.2)

✓ **Namna halisi**

✓ **Namna hili**

✓ **Namna vikariri**

✓ **Namna viigizi**

✓ **Namna ki-mfanano**

✓ **Namna kitumizi/ala**

(Nusu maki kila moja)

f) Tambuliza kivumishi kitenzi na kielezi katika sentensi hii

(Ala.3)

Mwalimu angali mgonjwa hata kama amekuwa akifunza darasani

Angali – kivumishi

Amekuwa – kisaidia

Akifuza – kikuu

Darasani - kielezi

g) Maneno yafuatayo yako katika ngeli gani?

(Ala.3)

a. Nyingu **A – WA**

b. Neno **L – YA**

c. Kizibo **KI - VI**

d. Onyesh matumizi ya kiakifishi cha kitone

(Ala.2)

✓ **Mwisho wa sentensi**

✓ **Kufupisha maneno**

✓ **Katika hesabu**

✓ **Kutenga shilingi na senti**

✓ **Kuandika tarehe**

✓ **Kutenganisha saa na dakika**

e. Andika kinyume cha sentensi hii

(Ala.2)

Juma alimwoa Farida mwaka jana

Juma alimtaliki Farida mwaka jana

- f. Kanusha sentensi hii
Ukinichapa nitakushtaki
Usiponichapa sitakushtaki
- g. Eleza maana ya sentensi ambatano (Ala.1)
Ni sentensi ambayo ina vishazi huru viwili na huunganishwa ni kiunganishi

ISIMU JAMII (Ala.5)

- a) Taja sifa tano za sajili ya michezo (Ala.5)
- ✓ **Lugha changamfu**
 - ✓ **Hutumia chuku katika maelezo**
 - ✓ **Hutumia lugha sanifu**
 - ✓ **Lugha ya jazanda**
 - ✓ **Lugha hujaa vijalizo**
 - ✓ **Msamiati unaovutia**
 - ✓ **Istilahi maalum za kimchezo**
 - ✓ **Hutumia ya utohozi**
 - ✓ **Kuchanganya msimbo**
 - ✓ **Lugha ya uwasifu**

FASIHI SIMULIZI (Ala.5)

- a) Vitendawili ni nini?
- ✓ **Ni semi ambayo ina maana fiche na uhitaji kufumbuliwa**
- b) Eleza majukumu manne ya vitendawili (Ala. 4)
- ✓ **Huelimisha jamii**
 - ✓ **Huchemsha bongo**
 - ✓ **Hukosa ufasaha wa lugha**
 - ✓ **Hukuza uwezo wa kukumbuka**
 - ✓ **Hudhihaki na kukejeli tabia hasi**
 - ✓ **Huleta umoja na ushirikiano katika jamii**
 - ✓ **Huchochea tabia ya udadisi**